

# جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

## مَشْرُوعُ تَعَلُّمِ الْإِسْلَامِ – أَصُولُ الْعَقِيدَةِ - سَوَاحِيْبِي

Samo la 12

الدرس الثاني عشر

### 2 : NGUZO YA PILI NI KUAMINI MALAIKA WA ALLAH.

Inakusanya nguzo hii kuwaamini malaika wote kwa pamoja na kuamini Malaika hawa kwa ufafanuzi zaidi.

Ama kuamini malaika wote kwa pamoja, ni kuamini ya kwamba mwenye zi mungu anao malaika aliowaumba kwa ajili ya kumtii yeye, na hao malaika wako aina nyingi, miongoni mwao ni;

- Malaika wanaobeba A'arsh ya Allah
- Malaika wa peponi na motoni
- Malaika waliowakilishwa kwa kuhifadhi matendo ya waja wake Allah.

Ama katika njia ya ufafanuzi, tunaamini ya kuwa wale aliowaita majina yao Allah na Mtume wake kama vile Malaika Jibril, Mikail, na Malaika Mwenye kumiliki khazina za Motoni, Israfil aliye wakilishwa katika kupuliza parapanda.

Na malaika hawa Allah amewaumba kwa nuru kama ilivyothibiti kutoka katika Hadithi ya mama Aisha mkewe Mtume Muhammad (saw) aliyopokea Imamu Muslim, Mtume (saw) anasema :

كما ثبت عن عائشة - رضي الله عنها - أن النبي - ﷺ - قال: «أُخْلِقتُ الملائكة من نور، وأُخْلِقتُ الجن من نار، وأُخْلِقتُ آدم مما أُوصِفَ لكم» [الرواسيل: ٢٩٩].

("Wameumbwa Malaika kwa Nuru na wameumbwa Majini kutokana na ndimi za moto na ameumbwa Adam kutoka na yale mliyoelezewa").

### 3 : NGUZO YA TATU NI KUAMINI VITABU VYA ALLAH.

Ni wajibu kuamini moja kwa moja ya kuwa mwenyezi mungu ameteremsha vitabu kwa manabii wake na mitume wake ili kubainisha haki kwa waja wake na kulingani kwa kutumia hivyo vitabu.

Tuamiani katika njia ya ufafanuzi kwa yale aliyoyasema mwenyezi mungu, miongoni mwa vitabu hivyo ni Taurat, Injili, Zabur na Quran, na Quran ndio kitsbu cha mwisho kuteremshwa, kimekuja kulia nguvu na kuvisadikisha vitabu vilivyo tangulia'

Kwa hiyo ni wajibu kwa watu wote kuifuata Quran na kuitolea hukumu katika mambo yao yote na kutumia yale yote yaliyo kuwa sahihi katika mafundisho ya Mtume Muhammad (saw), kwani mwenyezi mungu amemtumiliza Muhammad mtume kwa viumbe wa aina mbili (Athaqalaini- Majini na Binadamu) na akateremshiwa hii Quran ili awahukumu baina yao.

Mwenyezi mungu akaifanya Quran kuwa ni pozo (dawa) kwa yale yote yaliyomo vifuani mwa waja na niufafanuzi wa kila kitu, na ni muongozo na ni rahma kwa watu wote, Allah anasema:

قال تعالى: ﴿وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾ [الأنعام: ١٥٥]

("Na hiki kitabu tumekiteremsha kimebarikiwa, basi kifuateni na mcheni mwenyezi mungu ili mpate kurehemewa") (Al - An'am:155).

وقال سبحانه: ﴿وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَانًا لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ﴾ [النحل: ٨٩].

("Tumekuteremshia kitabu uwe ni upambanuzi wa kila jambo na ni muongozo na ni rahma na bishara njema kwa waislamu") (An-nahl: 89).

### 4: NGUZO YA NNE YA IMAANI NUKUAMINI MITUME WA ALLAH.

Ni wajibu kuwaamini Mitume wote kwa pamoja na kwa kupambanuzi, tuamini ya kwamba Allah (sw) amewatuma Mitume kwa waja wake, kwani Mitume ni wenye kubashiria watu mambo mema na kuwaonya watu na mambo maovu wao ni walinganiaji kwenye haki.

قال تعالى: ﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ...﴾ [النحل: ٣٦].

("Kwa hakika tulituma kwa kila umma mtume, kuwaambia watu wake wamuabudu mwenyezi mungu na wajepushe na twaghuti") (An-Nahl:36).

Mwenye kuitikia wito wa Mitume atafaulu na kusalimika, na mwenye kupinga wito wao ataa ngamia na kujuta.

Tunaamini kuwa ulinganiaji wa Mitume wote ni mmoja, nao ni ulinganiaji wa kumpwekesha mwenyezi mungu katika ibada, lakini waliitalafiana kwenye hukumu na sharia zao walizopewa na mwenyezi mungu.

Tunaamini kuwa wako Mitume bora kati yao, na mbora wao kati ya hao wote ni Mtume wa mwisho Muhammad (saw).

قال سبحانه: ﴿وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَى بَعْضٍ﴾ [الاسراء: ٥٥].

("Na kwa hakika tumewafadhilisha baadhi ya Mitume juu ya wengine") (Al Israh: 55).

وقال سبحانه: ﴿مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَكِنْ رَسُولَ اللَّهِ وَحَاتَمَ النَّبِيِّينَ﴾ [الأحزاب: ٤٠].

Allah (sw) anasema : (" hakuwa Muhammad ni baba wa mmoja katika waume zenu , lakini ni Mtume wa Mwenyezi mungu na ni mwisho wa Mitume") ( Al-Ahzab:40).

Na wale ambao Allah amewataja miongoni mwao au akathibitisha mtume wake majina yao, tunawaamini kwa ufafanuzi na kuelezwa kama vile mtume Nuhu, Hud, Swaleh, Ibrahim na wengineo pamoja na mbora wa Mitume Muhammad (saw).